

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Simu Na: +255 026 2321566
Nukushi: +255 026 2321514
Barua pepe: ps@mnrt.go.tz



Mtaa wa Kilimani,
Barabara ya Askari,
S.L. P 1351,
40472-DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Wizara ya Maliasili na Utalii inataarifu umma kuwa, taarifa iliyotolewa tarehe 09 Mei, 2018 na Taasisi ya Oakland iliyopo nchini Marekani ikiwa na kichwa cha habari **“Losing the Serengeti: the Maasai land that was to run forever”** na kunukuliwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza-BBC Swahili kwa kichwa cha habari **“Tanzania yadaiwa kukandamiza haki za Wamaasai wanaoishi Loliondo”** ni potofu.

Taarifa hiyo imeituhumu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa imefanya; uchomaji wa makazi kwa jamii ya wamasai, kuondoa mifugo yao kutoka kwenye maeneo ya malisho na maji, kuwatesa wananchi na kuwazuia kutoa maoni yao, taarifa ambazo si za kweli.

Ukweli ni kuwa, kutokana na umuhimu wa eneo hilo kwa uhifadhi, uwepo wa vyanzo vya maji, eneo la mzunguko wa uhamaji wa wanyamapori na maisha ya watu, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ilichukua hatua stahiki za kutatua mgogoro huo ikihusisha wadau wote muhimu yakiwemo mashirika yasiyo ya kiserikali, wawekezaji pamoja na wananchi.

Kazi hiyo inaendelea na Serikali itatoa taarifa rasmi kuhusu suala hili.

Wizara ya Maliasili na Utalii inawataka watanzania na jumuiya ya kimataifa kwa ujumla kupuuza taarifa hiyo potofu yenye lengo la kuipaka matope Serikali na kuleta uchonganishi baina yake, wananchi na wawekezaji kwa lengo la kuleta uvunjifu wa amani.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau wenye nia njema kwa uhifadhi na maendeleo ya wananchi katika kusimamia na kuendeleza rasilimali zilizopo katika eneo la Loliondo na maeneo mengine nchini kwa maslahi mapana ya Taifa.

A handwritten signature in green ink, reading 'Hamisi A. Kigwangalla'.

Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb)
Waziri wa Maliasili na Utalii
10 Mei, 2018